Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika
(WiLDAF)

# SHERIA YA NDOA, SURA YA 29 YA MWAKA 1971

# HAJA YA MABADILIKO YA KISHERIA

## Muhtasari wa Sera

Suala la: 2

Julai, 2021

Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika
(WiLDAF)

# SHERIA YA NDOA, SURA YA 29 YA MWAKA 1971

# HAJA YA MABADILIKO YA KISHERIA

## Muhtasari wa Sera

**Suala la: 2**

**Julai, 2021**

## MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU

- Kwa mujibu wa kifungu cha 114 cha Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019, kinaipa mahakama mamlaka ya kuagiza mgawanyiko wa mali ya ndoa pale ambapo wanandoa wataachana kwa kuzingatia mambo yaliyoanishwa katika kifungu hicho. Hata hivyo, kifungu hiki hakijaainisha haki za wanawake wengine kwenye ndoa za mitala.
- Wakati wa mgawanyo wa mali, kifungu cha 114 pia kinaitaka mahakama kuzingatia mila na desturi pamoja na kiwango cha michango iliyotolewa na kila mwenza kama fedha, mali au kazi wakati wa upatikanaji wa mali hizo.
- Kifungu cha 63 cha Sheria ya Ndoa kinachochea ukatili na ubaguzi kwa kutambua wajibu kwa mume pekee kumtunza mke wake kwa kumpa mahitaji yote muhimu katika maisha kama vile mavazi, chakula na malazi kulingana na uwezo wake. Mke analazimishwa Kufanya hivyo pale tu mume atakapokua hana uwezo wa kupata kipato kutokana na matatizo ya kiakili, ulemavu au ugonjwa.
- Kifungu cha 66 kinakataza mwenzi yeyote kumpiga mwingine kwa sababu yoyote, na kupigwa kwa mke ni moja ya sababu za kufungua jalada la talaka chini ya kifungu cha 97 na 107 (1). Hata hivyo, sheria ipo kimya juu ya adhabu itakayotolewa wakati mwenza mmoja anapompiga mwingine.
- Umri wa kisheria wa ndoa umewekwa kuwa miaka 15 kwa wasichana kwa idhini ya wazazi na 14 kwa idhini ya Mahakama huku kwa wavulana ikiwekwa umri wa miaka 18. Kifungu hiki kinachochea ubaguzi dhidi ya wasichana kupata elimu na kuwa na maamuzi juu ya mambo yanayohusu maisha yao.

## UTANGULIZI

Sheria ya Ndoa, Sura ya 29 ya mwaka 1971 kama ilivyorekebishwa mwaka 2019 ni sheria kuu inayosimamia maswala ya ndoa nchini Tanzania. Hata hivyo, imekabiliwa na changamoto nyingi ambazo ni pamoja na; inaruhusu mazingira fulani ya ubaguzi wa kijinsia. Kwa mfano, inawabagua wavulana na wasichana katika uwezo wa kuingia katika ndoa. Pili, Sheria ya Ndoa ina utata katika suala la ugawaji wa mali za ndoa wakati talaka hasa katika ndoa za mitala. Inatoa wajibu kwa mume tu kutoa mahitaji kwa ajili ya familia na imeshidwa kutoa adhabu kwa maswala ya ukatili hasa wa majumbani.

Muhtasari huu wa sera unaonyesha mapungufu na changamoto zilizopo katika sheria hii juu ya kusimamia maswala ya ndoa nchini Tanzania. Aidha, muhtasari huu pia unazungumzia haja ya kupitia na kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa Sura ya 29 ya mwaka 1971. Vile vile muhtasari huu zaidi unatoa mapendekezo yaliyozingatia hali ya sasa ya mambo ya ndoa katika nyakati za kisasa.

## SHERIA YA NDOA TANZANIA: UCHAMBUZI WA MUKTADHA

Mwaka 1971, Tanzania ilitunga Sheria ya Ndoa na kuwapa wanawake na wanaume haki kadhaa za msingi za kiraia juu ya ndoa na talaka., Sheria hii ni miongoni mwa sheria kongwe nchini Tanzania, na hivyo, inakabiliwa na changamoto nyingi katika suala la tafsiri. Mkanganyiko na migogoro mingi na sheria nyingine hasa zilizoundwa hivi karibuni kuendana na hali halisi kama vile Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, Miongozo na Mipango mingine ya Serikali. Sheria ya Ndoa ukatili dhidi ya wanawake na watoto nchini Tanzania.

Mwaka 2019, Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ilithibitisha uamuzi wa Mahakama Kuu katika kesi ya Rebeca Gyumi kuwa vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ni vya kibaguzi dhidi ya mtoto wa kike na ni kinyume na Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, vinapaswa kurekebishwa katika kipindi cha miezi 12, hata hivyo sheria ya ndoa, haijabadilishwa mpaka sasa. Aidha changamoto za sheria ya ndoa zinakwenda zaidi ya vifungu viwili tu vinavyoruhusu ndoa za utotoni.

Sheria ya ndoa nchini Tanzania kwa sasa imepitwa na wakati, haiendani na mambo mengi mapya ambayo yamejitokeza ndani ya miaka 50 ya utumikaji wake. Jamii yetu ya kisasa inastahili kuwa na sheria ambayo inawapatia wanandoa wote haki na uchaguzi wa jinsi ya kuishi pamoja na kutoa ulinzi dhidi ya unyanyasaji na ukatili ndani ya ndoa.

### Kwa nini Tanzania inahitaji Mageuzi ya Sheria ya Ndoa?

#### a) Ulinzi duni wa haki za wake wengine wakati wa talaka na mgawanyo wa mali katika ndoa za mitala

Sheria ya Ndoa inaruhusu ndoa za mitala. Hata hivyo kifungu cha 114 cha Sheria ya Ndoa, kinaeleza wazi kwamba mahakama ina mamlaka ya kuagiza mgawanyo wa mali pale wanandoa wanapopewa talaka. Katika kutumia mamlaka hayo mahakama itazingatia mambo kadhaa ikiwemo; Mila na desturi za wenza hao, kwa kiwango cha michango iliyotolewa na kila mwenza, kwa madeni yoyote kati ya wenza, na kwa mahitaji ya watoto wadogo, ikiwa yapo.

Kifungu hiki hakijazungumzia haki za wake wengine kwenye ndoa ya mke zaidi ya mmoja wakati mahakama ikigawa mali. Swali ambalo sheria hii haijalizungumzia ni Je, mahakama inapaswa kuzingatia mchango wa wake wengine ambao wanabaki kwenye ndoa baada ya mmoja wao kuomba talaka na mgawanyo wa mali? Ni taratibu zipi zitatumika kutambua mchango wa kila mmoja hasa katika

mgawanyo wa mali? Sheria ya Ndoa inapaswa kujibu maswali haya, kutokana na changamoto nyingi hasa katika utekelezaji wa sheria hii wakati wa mgawanyo wa mali kipindi cha talaka.

### b) Changamoto za tafsiri ya Dhana ya Ndoa

Kifungu cha 160 cha Sheria ya Ndoa, kinatoa muktadha wa Dhana ya Ndoa. Kwa mujibu wa kifungu hiki kuna dhana inayokanushika kuwa mwanamume na mwanamke wakiishi pamoja huweza kudhaniwa kuwa ni mke na mume mbele ya sheria japokuwa hawakuwahi kufunga ndoa. Kuthibitisha dhana hii ni suala la ushahidi ambao utatolewa na umma unaowazunguka kwamba unawachukulia na kuwapa heshima kama mke na mume. Dhana hii imenyima haki nyingi za wanawake hasa pale wanandugu wanaposhindwa kuwa tayari kutoa ushahidi juu ya dhana hiyo ya ndoa.

### c) Majukumu yasiyo sawa kati ya mume na mke ndani ya ndoa

Kifungu cha 63 cha Sheria ya Ndoa kinaweka wajibu kwa mume kumtunza mke wake kwa kumpa mahitaji yote muhimu katika maisha kama vile mavazi, chakula na malazi kulingana na uwezo wake. Mke pia atakuwa na jukumu hilo tu ikiwa mume hawezi kutekeleza / kutunza familia kwa sababu za ugonjwa hasa wa kiakili na ulemavu. Kifungu hiki ni baguzi hasa kwa wanaume ukizingatia dunia ya sasa inaelekea kwenye usawa wa kijinsia. Vile vile kifungu hiki kimehamasisha unyanyasaji dhidi ya wanawake kama wanaume wanavyodhani wanamiliki wanawake kama mali yao. Hii pia imesababisha utegemezi wa kiuchumi kati ya wanawake walioolewa. Sheria inapaswa kufafanua wazi kuwa na fursa sawa za kimajukumu kati ya mume na mke katika ndoa ili kuchochea wanawake wengi kujitokeza katika fursa za kiuchumi nk.

### d) Dhana ya kuthibitisha mchango wakati wa mgawanyo wa mali za ndoa wakati wa talaka

Sheria ya Ndoa inatoa haki ya kugawana mali za ndoa pale inapotokea wenza wametalakiana. Mali yoyote ambayo imepatikana wakati wa ndoa na mtu binafsi au mchango wa pamoja wa wanandoa inahitajika kugawanywa. Wakati wa mgawanyiko wa mali za ndoa, kuna mazoea ya kisheria ambayo wanawake tu wanapaswa kuthibitisha michango yao kwenye mali. Wakati mwingine wanatakiwa kutoa risiti za kuthibitisha mchango wao ambapo wakati mwingine ni vigumu sana kuthibitisha michango. Sheria inahitaji kufafanua wazi ugawaji wa mali ya ndoa na kufikiria kuruhusu kuanzisha mikataba ya umiliki wa mali binafsi kabla na baada ya ndoa.

### e) Mgongano wa Sheria katika kufafanua Tafsiri ya Mtoto

Kama ilivyoelezwa hapo awali, Sheria ya Ndoa ni sheria ambayo inasimamia maswala yote ya ndoa nchini Tanzania. Sheria ya Ndoa inapingana na sheria zingine ambazo zinafafanua tafsiri ya mtoto. Wakati Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, inamwelezea mtoto kama mtu mwenye umri chini ya miaka 18, Sheria ya Ndoa bado inamruhusu mtoto mwenye umri wa miaka 15 kuolewa kwa ruhusa ya wazazi. Tafsiri ya mtoto chini ya Sheria ya Mtoto haijabatilisha kifungu cha 13 ya Sheria ya Ndoa ambacho kinaweka umri wa chini wa ndoa kuwa miaka 15 kwa wasichana na 18 kwa wavulana. Mara kwa mara Serikali imekua ikikiri kwamba kushindwa kubadili kifungu hicho ni kutokana na unyeti wa kitamaduni na wa kidini juu ya jambo hilo.

Sheria ya Makosa Maalum ya Kujamiiana (SOSPA), 1998 ambayo sasa ni sehemu ya Kanuni ya Adhabu, inaweka umri wa ridhaa ya ngono kuwa miaka 18. Suala la ridhaa ya ngono halitumiki ikiwa msichana ameolewa chini ya umri wa miaka 18. Hii inaacha mianya kwa wengi kuepuka adhabu kwa sababu baada ya kutenda kosa, wengi hukimbilia kuoa watoto hao ili kukimbia mkono wa sheria na baadae kuwaacha au kuwapa talaka.

Uwiano wa sheria hizi ni muhimu linapokuja suala la kufafanua umri wa kuingia kwenye ndoa. Kuacha sheria hizi zikiwa zinakinzana kunafanya iwe vigumu kwa Serikali kutekeleza Mpango wake wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA-VAWC) 2016/17-2021/22, ambao unaitaka Serikali kwa kushirikiana na wadau kupunguza kuenea kwa ndoa za utotoni kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022.

### f) Ongezeko la Matukio ya Ukatili wa Majumbani

Sheria ya Ndoa iko kimya juu ya masuala yanayohusu unyanyasaji na ukatili wa majumbani; kuna ushahidi kwamba wanawake na watoto wengi nchini Tanzania wananyanyaswa na kunyimwa haki zao. Kifungu cha 66 cha Sheria ya Ndoa, kimegusia adhabu kwa wenza, kwamba hakuna mtu anayeruhusiwa kutoa adhabu ya viboko kwa mwenza wake, lakini kifungu hiki kinazuia tu unyanyasaji wa kimwili kati ya wanandoa, na kuacha aina nyingine za unyanyasaji ambayo ni pamoja na kihisia, kisaikolojia, ngono na kiuchumi.

### g) Sheria Kuruhusu Ndoa za Utotoni

Ndoa za utotoni ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu kwa wasichana. Sheria ya Elimu nchini Tanzania , ya mwaka 1978 kama ilivyofanyiwa marekebisho

mwaka 2016 inapiga marufuku ndoa za wanafunzi ; hata hivyo, sheria haijasema lolote kuhusu wasichana ambao hawako shuleni na kwa umri wao wangepaswa kuwa katika mfumo wa elimu. Sheria ya ndoa bado inaruhusu mtoto wa kike kuolewa na umri wa miaka 15. Tanzania bado haijafanya mapitio ya Sheria ya Ndoa ili kutoa ulinzi dhidi ya ndoa za utotoni, ingawa iliashiria kwamba itafanya hivyo. Pia, mipango kazi ya serikali ya kushughulikia ukatili dhidi ya wanawake na watoto haiweki mikakati ya kina kukabiliana na ndoa za utotoni. Takwimu za Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya (TDHS), 2015-2016 zilionyesha kuwa asilimia 36 ya mabinti wenye miaka 20 hadi 24 waliolewa kabla hawajatimiza umri wa miaka 18. Kwa mujibu wa Utafiti wa Demografia ya Afya nchini (TDHS) wa mwaka 2010 mikoa yenye viwango vikubwa vya ueneaji wa ndoa za utotoni hapa nchini ni Shinyanga (59%), Tabora (58%), Mara (55%) na Dodoma (51%). Hii ni sawa na kusema kuwa kwa wastani, wasichana wawili kati ya watano huolewa kabla hawajatimiza umri wa miaka 18.

### h) Dhamira ya Tanzania katika majukumu yake ya mikataba ya kimataifa

Kifungu cha 5 cha Itifaki ya Haki za Wanawake barani Afrika kwa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (unaojulikana kama 'Itifaki ya Maputo') kinakataza na kulaani aina zote za vitendo hatari ambavyo vinaathiri vibaya haki za binadamu kwa wanawake. Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto unamlinda mtoto dhidi ya mazoea mabaya ya kitamaduni kama vile ndoa za utotoni. Ndoa za utotoni ni ukiukwaji wa Ibara ya 16(2) ya Azimio la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, ambalo linasema: 'Ndoa itafungwa tu kwa ridhaa huru na kamili ya wanandoa waliokusudiwa.'

Kifungu cha 16 cha Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW) kinasema kuwa wanawake wanapaswa kuwa na haki sawa na wanaume "kuchagua mke kwa uhuru na kuingia katika ndoa tu kwa ridhaa yao kamili". Kwa kusaini Mkataba wa Haki za Mtoto (CRC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeahidi kuchukua "hatua zote madhubuti na zinazofaa na Kifungu cha 5 cha Itifaki ya Haki za Wanawake barani Afrika kwa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu. Zaidi ya hayo, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa yanatoa wito wa Usawa wa Kijinsia na Lengo la 5.3 hasa kutoa wito wa kuondoa mazoea yote mabaya ya kitamaduni ifikapo mwaka 2030, ikiwa ni pamoja ndoa za mapema na za kulazimishwa. Hii ni pamoja na , kukomesha mila za jadi zinazoathiri afya ya watoto, ambayo ni pamoja na, kati ya mazoea mengine, ndoa za utotoni.

Tarehe 23 Aprili , 2021 wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alipo hutubia Bunge, alisema kuwa serikali imedhamiria na imeweka kipaumbele chake katika kupunguza vifo vya akina mama wajawazito. Ikiwa wasichana walio chini ya umri wa miaka ishirini wanachangia karibu asilimia 20 ya vifo vya kina mama, kufikia malengo hayo itahitaji kuchukua hatua zinazofaa katika kushughulikia ndoa za utotoni na mimba za utotoni.

### i) Kukosekana kwa ulinzi wa watoto walioko nje ya mfumo wa elimu.

Kama ilivyoelezwa hapo awali Sheria ya Elimu nchini Tanzania inalinda wanafunzi wa shule wasiolewe na kuoa. Sheria haitoi ulinzi kwa wasichana wa nje ya shule dhidi ya ndoa za utotoni au mimba. Hakuna jitihada za kutosha kuwalinda watoto walio hatarini kuingia kwenye ndoa za utotoni na za kulazimishwa na kuwasaidia wahanga na msaada wa kisaikolojia, kijamii au kiuchumi ambao wanauhitaji sana. Mara nyingi wahanga wanahangaika na matokeo ya unyanyasaji waliotendewa, wakiwa peke yao. Zaidi ya hapo, wanapata msaada mdogo ili kufidia elimu yao waliyoipoteza au kuwasaidia kuandaa fursa za kujitunza wao wenyewe na watoto wao. Wakati baadhi ya vikundi vidogo na mashirika ya msaada ya kimataifa wanaendesha mipango, jitihada zao hazitoshi kufidia kushindwa kwa asasi za kiserikali kupitisha mikakati ya kitaifa ya kushughulikia mahitaji mbalimbali ya wahanga.

## MIFANO BORA KUTOKA NCHI NYINGINE ZA AFRIKA

**Rwanda**: Sheria inayohusiana na taasisi ya ndoa, uhuru, na urithi inatambua haki ya msichana kwa kurithi mali ya familia. Aidha, sheria hiyo imeweka umri wa miaka 21 kama kigezo cha idhini muhimu na uhalali wa ndoa, kufungwa. Sheria hii imekuwa na mchango mkubwa katika kupunguza ndoa za utotoni nchini Rwanda. Mathalani utafiti kutoka katika Shirika la Kimataifa la Watoto Duniani UNICEF (2017) wenye kichwa cha habari 'Kufikia Siku zijazo bila Ndoa za Utotoni'; Mtazamo juu ya Afrika Magharibi na Kati; unaonyesha kuwa nchini Rwanda ndoa za utotoni kabla ya umri wa miaka 15 ni asilimia 0%, wakati kiwango cha ndoa kabla ya umri wa miaka 18 ni 7%. Aidha, repoti hiyo imeonesha kuwa kuanzia mwaka 1990 hadi 2019 kuna upungufu wa ndoa za utotoni kwa asilimia 62 kutoka asilimia 18 hadi asilimia 7.

**Ghana:** Ghana imefanya juhudi za kisheria kuboresha mfumo wa ndoa ili kupunguza ndoa za utotoni. Nchini Ghana ni marufuku kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi. Vile vile, katiba ya Ghana ya mwaka 1992 imetamka bayana kuwa mtoto ni mtu mwenye umri wa miaka 18 na hivyo hawezi kuoa au kuolewa. Hii imesisitizwa na Sheria ya Watoto ya mwaka 1998, ambayo inaweka umri wa kisheria wa ndoa kuwa ni miaka 18 kwa wavulana na wasichana. Hatua zilizochukuliwa kushughulikia ndoa za utotoni nchini Ghana zinadhihirisha na kushuhudia jinsi marekebisho ya sheria yanayohusiana na ndoa yanaweza kuwa chombo muhimu cha kusaidia kushughulikia vitendo vya ndoa za utotoni. Matokeo ya utafiti wa UNICEF 2017 yanaonyesha kupungua kwa asilimia 40 katika ndoa za utotoni nchini Ghana kutoka 35% katika mwaka 1990 hadi 21% katika mwaka 2015.

**Malawi**: Malawi ni moja ya nchi zenye viwango vya juu vya ndoa za utotoni duniani, ambapo msichana mmoja kati ya wasichana wawili anaolewa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18 (UNFPA 2012). Mnamo Februari 12, 2015, Bunge la Malawi lilipitisha Muswada wa Ndoa, Talaka na Uhusiano wa Familia (Sheria ya Ndoa). Sheria hiyo ilitiwa saini mwezi Aprili 2015 na Rais Peter Mutharika. Kupitiwa na kupitishwa kwa Sheria ya Ndoa mpya imekuwa hatua muhimu katika kupata haki za wanawake na wasichana katika nchi ambayo mila na mfumo dume zimeingizwa sana, umaskini umeenea, na wasichana kwa ujumla wana nafasi ndogo juu ya viashiria vya maendeleo. Sheria mpya ya Ndoa inaimarisha utawala wa ndoa nyingi na kushughulikia vipengele vya kibaguzi katika sheria zilizopita zilizokua zinasimamia ndoa na mahusiano ya kifamilia. Kifungu kilichovutia zaidi ndani na kimataifa ni sheria hiyo kuweka umri wa ndoa kuwa ni miaka 18 na

kuhitaji usajili rasmi wa serikali wa ndoa zote ili kubaini ndoa za utotoni haraka na kuchukua hatua.

## Mapendekezo ya Sera na Mipango

### Wito kwa Watunga Sera na Watendaji wa Kisheria:

1. Kupitia upya na kufanya maboresho ya Sheria ya Ndoa ya Tanzania, ya mwaka 1971 na kuweza kushughulikia kasoro zote zinazojitokeza hasa katika masuala ya kutengana, talaka, ukatili nk. Jitihada zifanyike kupatanisha sheria ili kuweka uwazi na usawa kwenye utekelezaji kwa kurekebisha sheria na kuweka mambo yote yanayohusu ndoa na familia katika Sheria ya Ndoa. Sheria ya Ndoa itamke wazi mambo yafuatayo;
    - ✓ Inaweka kwa uwazi umri mdogo wa kuoa au kuolewa kwa wavulana na wasichana kuwa miaka 18.
    - ✓ Inatambua usawa wa ndoa zote, inahakikisha usawa wa haki ya kuolewa au kuoa, usawa kwenye ndoa, na wakati wa kuachana kwa wanandoa wote; na inatambua usawa wa haki hizi kwenye ndoa zote. Haki hizi zinapaswa kujumuisha haki ya kumiliki na kurithi mali, na hifadhi ya watoto.
    - ✓ Inaweka wazi vigezo vya ridhaa huru ya wenza wote kuoa au kuolewa, na inaondoa uhitaji wa ridhaa ya wazazi kwa ndoa kufungwa.
    - ✓ Inaweka uthibitisho wa umri kuwa ni lazima kwa ndoa kufungwa.
    - ✓ Inafanya uandikishaji wa ndoa kuwa ni lazima.
    - ✓ Inaweka wazi adhabu kwa watu wazima wanaohusika kwenye kupanga, kufungisha na kuandikisha ndoa za utotoni au ndoa za kulazimishwa.
    - ✓ Inaweka adhabu zilizo wazi kwa vitendo vya kikatili dhidi ya wanawake na Watoto kama ukatili wa kimwili, kiuchumi, kisaikolojia, kingono na aina nyingine vinavyofanyika katika ngazi ya familia
    - ✓ Inalinda haki na hadhi za wanawake waliokuwa kwenye ndoa za mke zaidi ya mmoja hasa wakati wa mgawanyo wa mali.
2. Serikali ifanye jitihada katika kuzifuta sheria zote zinazobagua wanawake na watoto pamoja na ndoa za utotoni hasa zile zinazoruhusu matumizi ya sheria ya kimila kwenye mambo ya ndoa, talaka, na mirathi.

3. Serikali ichukue hatua muhimu ili kutunga sheria ya kina dhidi ya ukatili wa majumbani kwa kufanya ukatili wa majumbani kua kinyume na sheria na hivyo adhabu kali itolewe.

### Wito kwa Serikali, Mashirika ya Kiraia, na Vyombo vya Habari:

- Serikali kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia kuboresha hali ya kiuchumi ya wasichana na wanawake kwa kutekeleza majukumu sawa na kupunguza umaskini ambao husababisha ndoa za utotoni.
- Wadau wa maendeleo kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia zinapaswa kuanzisha kampeni ya kitaifa ya kupunguza na hatimaye kukomesha ndoa za utotoni kama ilivyopendekezwa katika Utafiti wa Taifa wa Ndoa za Utotoni (2017).
- Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA), ngazi za kata na vijiji zinapaswa pia kushiriki kutokomeza ndoa za utotoni kwa kupitia kamati za Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA VAWC 2017/18 -2021/22).
- Kuandaa mipango mikakati ya kuwawezesha wasichana na wanawake na kuanzisha uhamasishaji wa jamii na unaojaribu kuwashawishi wazazi, kaya na viongozi wengine wa jamii kuepuka mazoea yanayozuia ustawi wa wanawake katika ndoa na athari za ndoa za mitala.
- Kushirikisha wanaume na wavulana kwenye kuchukua hatua dhidi ya ukatili na unyanyasaji hasa wa kwenye ndoa.
- Vyombo vya habari vipaze sauti kukemea matukio yanayopinga usawa wa kijinsia hasa katika ndoa na familia kwa ujumla.

### Kuhusu Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo BaraniAfrika (WiLDAF)

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika, ni mtandao wa mashirika ya watu binafsi katika Bara la Afrika ambao unafanya kazi za kupinga haki za wanawake, kujitolea kukuza na kuimarisha mikakati inayounganisha sheria na maendeleo ili kuongeza ushriki wa ushawishi wa wanawake katika mikakati na pia kueneza chachu hiyo katika ngazi ya jamii, kitaifa na kimataifa.

WiLDAF ilisajiliwa nchini Tanzania mnamo mwaka 1997 chini ya Sheria ya Makampuni Sura ya 212 kama Shirika lisilo la kiserikali, lisilo la kisiasa na lisilojiendesha kwa faida.

WiLDAF Tanzania ina njozi ya kuona jamii ya Tanzania inayoheshimu haki za binadamu za wanawake. Misheni ni kujenga ni kujenga mtandao imara kwa ajili ya kukuza heshima kwa haki za binadamu za wanawake kupitia utetezi, usambazaji na uangalizi wa vyombo mbalimbali vya kitaifa na kimataifa pamoja na mpango wa dharura wa kuitikia ukatili wa kijinsia katika ngazi zote wakati huo huo ikihusisha shseria na maendeleo.

## Kuhusu Mradi wa Uchechemuzi kwa Kutumia Takwimu (DDA)

Mradi wa uchechemuzi kwa kutumia Takwimu (DDA) ni mradi unaofadhiliwa na Shirika la Kimataifa liitwalo Freedom House pamoja na PACT Tanzania.

Mradi huu ambao ni wa miaka mitano unakusudia pamoja na mambo mengine kutumia takwimu kama sehemu ya kushawishi mabadiliko ya Sera na Sheria ambazo zinalinda na kutetea haki za binadamu.

Mradi huu unafanya kazi kwa kupitia vikosi kazi (WGs) mbalimbali. WiLDAF inaratibu kikosikazi namba mbili (WG2) ambacho kimejikita katika kusimamia haki za Wanawake,Watoto, Vijana na watu wenye ulemavu

## SHUKRANI

Taarifa hii fupi ni mchango wa watu binafsi, mashirika na wanachama wa kikosi kazi namba 2 ambao kwa pamoja wameshiriki katika kuandaa taarifa hii.

Kwa niaba ya kikosi kazi namba 2 (WG2), WiLDAF inapenda kutambua juhudi iliyofanywa na muandishi Bwana Idd Rajabu Mziray kwa kujitolea kwake katika kuandaa rasimu ya awaliya taarifa hii fupi.

Vile vile tunatoa shukrani kwa Mkurugenzi wa WiLDAF Anna Kulaya kwa kuhariri taarifa hii fupi.

WiLDAF inapenda kuwashukuru wafuatao kwa kupitia na kuchangia katika kuboresha taarifa hii fupi; Bi Zakia Msangi, Bi Miriam Azaria, Asajile Mwakyusa, Simoni Songeraeli, Michael Lwakatare pamoja na Bi Anneth Mushi.

Mwisho, shukrani ziende kwa wanachama wa WG2 ambao wameshiriki kikamilifu katika kuandaa taarifa hii fupi kama ifuatavyo;

1. Women in Law and Development in Africa (WiLDAF),
2. Tanzania Child Right Forum (TCRF),
3. Tanzania Domestic Workers Coalition (TDWC),
4. Mwanza Children and Youth Network (MCYN),
5. Tanzania Early Childhood Development Network (TECDEN),
6. Zanzibar Female Lawyers Association (ZAFELA),
7. Tanzania Association for children Advancement (ZACA),
8. Women Legal Aid Centre (WLAC),
9. Women with Disability Network (SHIVYAWATA),
10. Youth Partnership countrywide (YPC),
11. Gender and Adolescence Initiative (GAI)
12. Vijana Pambana Pata Maendeleo Rukwa (VIPAMARU),
13. Jitambue Lembuka,
14. Health Integrated Multispectral Services (HIMS),
15. Women Development for Science and Technology Association (WODSTA).

## MAREJEO


1. Avalos, L., et al. 2015 'Kukomesha ukeketaji wa na ndoa za utotoni nchini Tanzania(Inapatikana kupitia http://www.azaniapost.com/education/parents-concerned-aboutban-on-school-contributionsh12674.html

2. **Jukwaa la** Utendaji la **Beijing**. 1995. Hatua ya Usawa, Maendeleo na Amani. Mkutano wa nne wa dunia kuhusu wanawake. Bejing, China. Inapatikana kutoka http://bit.ly/1Trml7D

3. **CHRR. 2011;** "Ripoti mbadala ya Mapitio ya Jamhuri ya Malawi na Kamati ya Haki za Binadamu, Kituo cha Haki za Binadamu na Ukarabati. Inapatikana kwa: http://bit.ly/1p1lVYN

4. ICRC, 2018: "Athari za kiuchumi za ndoa za utotoni: matokeo muhimu julai 2018)

5. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii. Jinsia, Wazee na Watoto. 2017. 'Utafiti wa Taifa kuhusu vichocheo na Matokeo ya Ndoa za Utotoni Tanzania'. Inapatikana katika: http://www.mcdgc.go.tz/data/national_survey_ [imepitiwa 8 Machi, 2018].

6. Mutyaba, R. 2011. 'Ndoa za mapema: ukiukwaji wa haki za msingi za wasichana barani Afrika', Jarida la Kimataifa la Haki za Watoto, 19(2): 341.

7. Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP). 2001. Ripoti ya Ufuatiliaji wa VVU / UKIMWI / STI Nambari 16. Dar es Salaam: Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, Wizara ya Afya. http://www.nacp.go.tz/site/publications/epidemiology-and-research-uratibu

8. Rebecca Gyumi v. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Misc. Civil Cause no. 05 ya 2016. Rutgers Tanzania 'Haki ya kutoa elimu kwa wasichana wajawazito na kina mama vijana. Inapatikana kwa: https://www.rutgers.international/sites/rutgersorg/files/PDF/Advoca cy_Tanzania_0.pdf

9. Human Right Watch "Ndoa za Utotoni: Tanzania" Agosti 2014

10. Kamati ya Umoja wa Mataifa ya kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake (1992). Mapendekezo ya Jumla ya CEDAW Na. 19 juu ya Unyanyasaji dhidi ya Wanawake (Kikao cha 11), Geneva: Umoja wa Mataifa. Inapatikana kwa: http://www.refworld.org/docid/52d920c54.html

11. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. 2015. Utafiti wa Viashiria vya Idadi ya Watu na Afya Tanzania na Utafiti wa Viashiria vya Malaria (2015-16 TDHS-MIS)

12. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. 2016. Mpango kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (NPAVAWC 2017/18 – 2021/22)

ISBN 978-9912-9860-1-5

**Imechapishwa na WiLDAF, 2021**
Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo barani Afrika
Eneo la Mikocheni A. Mtaa wa WiLDAF, Block F. Ploti Na. 635.
S.L.P 76215, Dar es salaam, Tanzania

**Simu:** +255222701995,
**Barua pepe:** wildaftanzania@gmail.com / info@wildaftanzania.or.tz
**Tovuti:** www.wildaftanzania.or